Barry, A. L. - WHAT ABOUT? LIVING TOGETHER WITHOUT MARRIAGE - *Swahili*

Kuhusu Jambo Gani...

# Kuishi Pamoja Kabla Ya Ndoa

**Daktari A. L. Barry**
**Rais**
**Kanisa la Kilutheri la Sinodi ya Missouri**

Kuna ongezeko la wasichana na wavulana wanaochagua kuishi kama mume na mke kabla ya ndoa. Kabrasha hili litajibu baadhi ya maswali yanayoulizwa juu ya kuishi pamoja kabla ya ndoa.

**Ndoa ni Nini?**

Neno la Mungu linatufunza kwamba, ndoa ni kuishi pamoja mpaka kufa, mwambatano wa pekee kati ya mume mmoja na mke mmoja kama bwana na bibi. Ndoa ni sehemu ya uumbaji wa Mungu. Hivyo, tunasoma katika Neno Lake, yaani, Biblia: "Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja" (Mwa. 2:24; linganisha na Mat. 19:5-6; Efe. 5:31).

Kwingineko tunasoma, "Lakini kwa sababu ya zinaa kila mwanamume awe na mke wake mwenyewe, na kila mwanamke awe na mume wake mwenyewe" (1 Kor. 7:2). Tena, "Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu" (Ebr. 13:4). Ndoa ni baraka ya thamani sana, kwa kuwa Mungu alimvuvia Mtume Paulo ili aielezee kama taswira ya uhusiano kati ya Kristo na biarusi Wake, yaani, Kanisa (Efe. 5:22-23).

**Kwa Nini ni Kosa Mtu na Mkewe Kuishi Pamoja kabla ya Ndoa?**

Inatajwa hasa kwamba, ni kutenda dhambi kwa mtu na mkewe kuishi pamoja kama bwana na bibi kabla ya ndoa. Neno la Mungu li wazi: "Tangu sasa msienende kama Mataifa waenendavyo, katika ubatili wa nia zao; ambao; akili zao zimetiwa giza, nao wamefarikishwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao . . . wakiisha kufa ganzi wanajitia katika mambo ya ufisadi wapate kufanyiza kila namna ya uchafu kwa kutamani" (Efe. 4:17 19). Wakati mmoja, Bwana wetu Yesu Kristo alimsaidia mwanamke aliyeishi na mtu ambaye hakuwa mumewe atambue kwamba, alilolitenda lilikuwa kosa (Yohana 4:16-18).

Wakristo Walutheri huamini kwamba, amri ya sita, "Usizini," humaanisha, "Imetupasa kumwogopa na kumpenda Mungu, ili kuwa na maisha matakatifu na safi katika maneno na matendo, kila mmoja akimpenda na kumheshimu mke wake au mume wake." (Katekisimo Ndogo ya Luther [CPH: 1986], uk. wa 15).

Haya yote ni namna nyingine ya kuyataja yaliyo wazi: Wasichana na wavulana hawapaswi kuishi pamoja kama mtu na mkewe isipokuwa wawe bwana na bibi. Hili ni kweli kwa wenye umri wa miaka (80) sawasawa na ilivyo kweli kwa wenye umri wa miaka (18).

**Kwa Nini Kanisa Liyajali yale Watu Wazima Wawili Wamekubaliana Kuyatenda?**

Kanisa linajali kwa sababu Mungu hujali. Neno la Mungu li wazi kabisa kuhusu hukumu ya kujamiiana nje ya ndoa. Zisome aya zifuatazo:

"Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi" (1Kor. 6:9-10).

"Lakini uasherati usitajwe kwenu kamwe, wala uchafu wo wote wa kutamani, kama iwastahilivyo watakatifu" (Efe. 5:3).

"Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu ufusadi, ... katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo

hawatarithi ufalme wa Mungu" (Gal. 5:19-21).

**Kwa Nini Kuishi Pamoja [kabla ya ndoa] ni Tatizo Nyeti Hivyo?**

[Kuishi pamoja kabla ya ndoa ni tatizo nyeti] kwa sababu Neno la Mungu huonyesha waziwazi kwamba, ni dhambi kwa mtu na mkewe kuishi pamoja kabla ya ndoa. Watu wanaoendeleza tabia ambayo Mungu huikataa na kuihukumu kama dhambi wanachagua njia ambayo inaweza kuwapeleka katika adhabu ya milele. Neno la Mungu ni wazi: "Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi" (Ebr. 10:26).

Na tena tunasoma: "Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu, mwepukane na uasherati; kila mmoja wenu ajue kuuweza mwili wake katika utakatifu na heshima; si katika hali ya tamaa mbaya, kama Mataifa wasiomjua Mungu . . . Bwana ndiye alipizaye kisasi cha haya yote; kama tulivyowaambia kwanza, tukashuhudia sana. Maana Mungu hakutuitia uchafu, bali tuwe katika utakaso" (1 The. 4:3-7).

**Je, si Kanisa Linakuwa 'lenye Kuhukumu'?**

Kanisa linatangaza kweli ya Neno la Mungu. Kwa niaba ya Kristo na watu Wake, wachungaji wana jukumu la kuwazungumzia waziwazi waume na wake wanaoishi pamoja [kabla ya ndoa] na kuwahubiria Neno la Mungu, yaani, Sheria na Injili. Si rahisi kwa mchungaji au usharika, kuwachukulia hatua waume na wake wao wanaoishi pamoja kabla ya ndoa. Ni muhimu kwa wachungaji na sharika kuzichukulia hatua hali hizi kiuchungaji na kwa uaminifu, kwa kujali. Waume na wake wao, wazazi wao, wanajaribiwa kusema, "Kwa hiyo? Si kila mtu hufanya hivyo; na isitoshe, tunaishi wakati tofauti." Katika kuihubiri kweli ya Neno la Mungu juu ya hali hizi, kanisa huwa aminifu, si lenye kuhukumu.

**Si Inampasa Mume na Mkewe Kuona kama Watatangamana?**

Utafiti duniani umeonyesha kwamba, matokeo ya kuishi pamoja kabla ya ndoa huwa ni mahusiano yasiyokuwa imara na yasiyokuwa matimilifu kuliko yale ya ndoa. Isitoshe, waume na wake wanaoishi pamoja wana hatari kubwa ya kutalikiana wakati wataoana hatimaye. Kuishi pamoja [kabla ya ndoa] ni tendo baya, hata kutoka katika mtazamo kamili wa kibinadamu.

Uchunguzi mmoja husema, "Wale wanaoishi pamoja kabla ya ndoa wana nafasi kubwa ya kutalikiana kuliko wale wasioishi pamoja; tofauti iliyorekodiwa ikiwa ni kati ya asilimia 50% mpaka asilimia 100% zaidi (The Relationship Between Cohabitation and Divorce" [1992], Demograghy, 29:357 374). Uchunguzi uliofanywa katika vyuo vikuu vya Yale na Columbia uligundua kwamba, "Kwa wastani, kiwango cha kuachwa kwa wanawake wanaoishi na wale watakaokuwa mabwana wao wa siku zijazo ni karibu asilimia 80% zaidi ya viwango vya wale wasioachwa ("Commitment and the Modern Union," American Sociaological Review, [1988], 53:127-138).

**Kanisa Linazichukulia Hali Hizi Hatua Gani?**

Kanisa na wachungaji wake, watawajulisha waume na wake wao wanaoishi pamoja kabla ya ndoa kwamba, wanalolitenda ni dhambi. Mazungumzo haya yatafanywa kwa njia ya upendo; lakini inapasa yafanywe kwa uaminifu wa Neno la Mungu. Hali hizi haziwezi kupuuzwa au

kutotiliwa maanani. Itawezekana kuwalazimisha waume na wake wao wanaoishi pamoja kabla ya ndoa kuwekwa chini ya marudi ya kanisa ili kuwasaidia watambue ubaya wa hali hii.

Hatua kama hii inaweza kuwakasirisha watu. Wanaweza kulikasirikia kanisa, au mchungaji wa kanisa. Wakati mwingine, familia nzima inapinduliwa wakati hali waliyokwisha kuipuuza inachukuliwa hatua hatimaye. Neno la Mungu lina njia ya kuyapitia mambo yote na kufichua hali yetu yenye dhambi. Hiyo ni kazi ya Sheria ya Mungu, inayotuonyesha dhambi yetu. Naam, lengo la kanisa si kuwakasirisha watu, wala si tamaa ya kanisa tu kuwafanya watu watambue dhambi zao. Kanisa huwataka watu waone dhambi zao ili waweze kumwona Mwokozi wao. Kuitangaza Injili ndicho kipaumbele kikukuu cha kanisa. Kanisa hutangaza Sheria ya Mungu ili watu waweze kusikia na kuamini habari njema kwamba, "Na damu yake Yesu, Mwana [W[ake, yatusafisha dhambi yote" (1 Yoh. 1:7). Kanisa huwataka watu wasikie Injili, kwa kuwa Injili tu ndiyo ina nguvu kubadilisha maisha na tabia kwa ajili ya wema.

**Mume na Mkewe Wanaoishi Pamoja Wanawezaje Kuisuluhisha Hali hii?**

Mume na mkewe wanaoishi pamoja kabla ya ndoa huhitaji kuchukua hatua thabiti ili kuikomesha hali hii. Wanaweza kuamua kutengana, bila mipango yoyote ya ndoa. Wanaweza kuamua kutengana mpaka waoane karibuni.

Ni muhimu kwao kupokea ushauri juu ya ndoa kabla ya arusi yao, na labda pia baada ya arusi yao. Baadhi ya waume na wake wanaweza kuchagua kuoana mbele ya afisa wa mahakama. Kwa kanisa, hii ni ndoa halali kabisa. Waume na wake wao wanaochagua njia hii wanatiwa moyo wafanye ndoa yao itambuliwe na watu wa kanisa pia. Haidhuru uamuzi utakavyokuwa, watahitaji ushauri wa mchungaji wao.

Nini Suluhisho la Mwisho la Tatizo Hili?

Kuna masuluhisho mengi tunayoweza kuyatambua. Familia za Kikristo zinahitaji kufahamu lililo jema na lisilo baya. Wazazi wanahitaji kuwazungumzia wanao mapema kuhusu matarajio ya Mungu juu ya ndoa.

Wachungaji na sharika zinahitaji kuwashughulikia waume na wake wao waliotenda dhambi hii. Sharika za Kikristo zinazojali huhitaji kuomba kwamba, Roho Mtakatifu atafanya kazi mioyoni na maishani mwa hao wanaoishi maisha haya ili kuuharibu upinzani wao kwa Neno la Mungu. Sharika za Kanisa lazima zisilipuuze tatizo hili, bali lazima zilishughulikie kwa uaminifu. Sharika zinahitaji kulizungumzia jambo hili.

Waume na wake wao wanaotambua dhambi yao huhitaji kulisikia Neno la kufariji la ahadi ya Mungu: "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yoh. 1:9). Wakiamua kuoana, inawapasa kufanya hivyo kwa tumaini lenye furaha katika msamaha wa Mungu na baraka Zake katika ndoa yao.

Daktari A. L. Barry
Rais
Kanisa la Kilutheri la Sinodi ya Missouri